

حرافين



رئاسة الشؤون الدينية  
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي

# NJIA ZENYE FAIDA KWA MAISHA YENYE FURAHA

Kiswahili

سواحيلي

الوسائل المفيدة للحياة السعيدة



Mwandishi

Abdur-Rahman Bin Nasir as-Sadi

جـ جمعية خدمة المحتوى الإسلامي باللغات ، ١٤٤٦ هـ

السعدي ، عبد الرحمن  
الوسائل المفيدة للحياة السعيدة - سواحيلي. / عبد الرحمن  
السعدي - ط١ . . - الرياض ، ١٤٤٦ هـ

٣٠ ص : .. سم

رقم الإيداع: ١٤٤٦/١٣٤٤٢  
ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٨٥١٧-٧٥-٨

# الوسائل المفيدة للحياة السعيدة

## NJIA ZENYE FAIDA KWA MAISHA YENYE FURAH

**Mtunzi:**

Sheikh, Abdurahman bin Naaswir Assa'adiy  
(Mwenyezi Mungu amrehemu)

(سواحلي)

## **Utangulizi wa Mwandishi**

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, ambaye sifa njema zote ni zake, na ninashuhudia kwamba hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu peke yake, asiyé na mshirika, na ninashuhudia kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume wake, na rehema na amani za Mwenyezi ziwe juu yake, jamaa zake na Maswahaba wake.

Ama baada ya hayo: Kwa hakika raha ya moyo, utulivu wake, furaha yake na kuondoka kwa msongo wa mawazo na huzuni, ndicho kitu ambacho kila mtu anakitafuta, na kwa hayo yanapatikana maisha mazuri, na inatimia furaha na bashasha kubwa. Hayo yana sababu za kidini, za kiasili na za kimatendo. Hata hivyo, hayo yote hayawezi kukusanyika pamoja isipokuwa kwa Muumini. Ama kwa wengine wasiokuwa Waumini, ingawa wanaweza kupata baadhi yake kwa njia na sababu fulani ambayo akili za watu wao wenye akili timamu zinapambana kuzifikia, bado wanayakosa kwa njia bora, thabiti na nzuri zaidi kwa hali na matokeo.

Lakini nitataja katika makala hii kile nitakachokumbuka mionganí mwa sababu za hitajio hili la hali ya juu ambalo kila mmoja analipupia.

Miongoni mwao, kuna wale waliofanikiwa katika mengi ya hayo, wakawa na maisha mazuri, wakaishi maisha yenyeye furaha. Na mionganoni mwao, kuna wale walioshindwa kabisa, wakawa na maisha ya taabu na yaliyo duni. Na mionganoni mwao kuna wale walio katikati, kulingana na kile walichowezeshwa kukifikia. Na Mwenyezi Mungu ndiye Muwezeshaji, na ndiye anayeombwa msaada wa kufikia kila heri na kupusha kila shari.

## Sura ya Kwanza

**1-** Sababu kubwa na asili ya hilo ni kuwa na imani na kutenda mema. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيهِ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنُجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾. [التحل: ٤٧]

*"Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, hakika tutamhuisha maisha mema; na hakika tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyokuwa wakiyatenda."* (An-Nahl: 97).

Hapa, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwapa habari na akawaahidi wale waliojumuisha

imani na matendo mema kwamba watakuwa na maisha mema hapa duniani, na malipo mema katika nyumba hii na katika nyumba ya maisha ya milele.

Sababu ya hilo iko wazi: Kwani, wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu imani iliyo sahihi, inayozalisha matendo mema yanayoboresha nyoyo, tabia, dunia na akhera, wanayo misingi ambayo wanapokea kwayo sababu zote zinazowajia, za furaha na shangwe, na pia sababu za wasiwasi, msongo wa mawazo na huzuni.

Wanapokea mambo wanayoyapenda na ya kufurahisha kwa kuyakubali, kushukuru na kuyatumia katika mambo yenye manufaa. Kwa hivyo, wanapoyatumia kwa njia hii, wanapata - kwa sababu ya kuyafurahia, kuwa na tamaa ya kudumu kwake na baraka zake, na kutarajia malipo ya wenyе kushukuru - mambo makuu yanayozidi kwa mema yake na baraka zake mambo haya ya furaha ambayo hayo ni matunda yake.

Na wanapokea machukizo, madhara, majonzi na huzuni kwa kukabiliana na yale wanayoweza kukabiliana nayo, na kupunguza yale wanayoweza kupunguza na kuwa na

subira nzuri kwa yale wasiyoweza kuepuka. Kwa njia hii, wanapata -kutoka kwa athari za machukizo hayo, kutokana na kukabiliana nayo kukabiliana kwenye manufaa, tajiriba na nguvu, na kutokana na subira na kutarajia malipo na thawabu - mambo makuu yanayofutilia mbali shida, na inachukua mahali pake, furaha, matarajio mema na matumaini ya kupata fadhila za Mwenyezi Mungu na malipo yake, kama alivyosema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuhusiana na hilo katika Hadithi sahihi:

«عَجَبًا لِأَمْرِ الْمُؤْمِنِ، إِنَّ أَمْرَهُ كُلُّهُ لَهُ خَيْرٌ، وَلَيْسَ ذَاكَ لِأَحَدٍ إِلَّا لِلْمُؤْمِنِ، إِنْ أَصَابَتْهُ سَرَّاءُ شَكْرٍ، فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَّاءُ صَبَرٍ، فَكَانَ خَيْرًا لَهُ». (رواه مسلم).

**“Linashangaza jambo la Muumini. Hakika mambo yake yote ni heri. Ikimpata heri, anashukuru, na hilo linakuwa ni heri kwake. Na likimtokea jambo haya, huwa na subira, na hilo linakuwa ni heri kwake. Na hili huwezi kulipata isipokuwa kwa Muumini tu.”** (Imepokelewa na Muslim).

Kwa hivyo, Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, akajulisha kwamba Muumini, kushinda kwake, heri yake

na matunda ya matendo yake yanazidishwa katika kila kinachompata cha kufurahisha na cha kuchukiza. Ndiyo maana unakuta watu wawili wamefikwa na jambo la heri au ubaya, na wanatofautiana sana katika kuitikia kwao, na hilo ni kulingana na tofauti zao katika imani na matendo mema.

Huyu ambaye ameelezewa kwa sifa hizi mbili anaipokea heri na shari kwa yale tuliyosema ya shukrani na uvumilivu na yale yanayofuatia. Hivyo, anapata furaha na shangwe, kuondoka kwa msongo wa mawazo, huzuni, wasiwasi, dhiki ya moyoni na ugumu wa maisha, na maisha yake yanakuwa mazuri hapa duniani.

Naye huyo mwingine, hupokea neema kwa uovu mkubwa, kiburi na dhuluma. Kwa hivyo, maadili yake yanapotoka na anaipokea kama vile wanyama wanavyoipokea kwa uchoyo na hofu, na bado moyo wake hauna amani. Bali unatawanyika katika pande mbalimbali. Unatawanywa katika upande wa hofu yake juu ya kutoweka kwa vitu avipendavyo, na kwa sababu ya upinzani mwangi ambao mara nyingi hujitokeza kutokana nayo, na kwa upande wa kwamba nafsi hazisimami kwenye

kikomo fulani. Bali husalia na shauku ya mambo mengine, ambayo yanaweza kutokea au yasitokee. Ikiwa yatatokea inavyotarajiwa na kukadiriwa, basi hilo pia ni wasiwasi tu kutokea zile pande zilizotajwa. Vile vile, wao hupokea matatizo kwa wasiwasi, hofu, na kulalamika. Kwa hivyo, usiulize juu ya kile kinachompata cha maisha ya taabu, magonjwa ya akili na mishipa ya ufahamu, hofu ambayo inaweza kumpelekea kwenye hali mbaya zaidi na mambo mabaya ziadi ya kumsumbu; kwa sababu hatarajii malipo yoyote, wala hana subira inayoweza kumfariji au kumrahisishia mambo hayo.

Yote haya yameshuhudiwa kwa uzoefu. Na mfano mmoja wa aina hii, ukiutafakari na kuutumia kwa hali za watu, utaona tofauti kubwa kati ya Muumini anayefanya matendo kwa mujibu wa imani yake, na yule asiyekuwa hivyo. Hilo ni kwa sababu dini inahimiza sana kutosheka na riziki ya Mwenyezi Mungu, na yale aliyowapa waja wake katika fadhila na ukarimu wake mbalimbali.

Muumini anapajaribiwa kwa maradhi, ufukara au matatizo mengine mionganoni mwa mambo ambayo yanampata kila mtu, basi yeye

- kwa imani yake na kwa alicho nacho cha kutosheka na kuridhia kile ambacho Mwenyezi Mungu alimgawia - anakuwa mwenye macho yaliyotulia, na hatafuti moyoni mwake jambo ambalo hakupangiwa, na anawatazama wale walio chini yake, wala hawatazami wale walio juu yake, na hata pengine furaha yake na bashasha yake inaweza kuzidi yule ambaye alipata mahitaji yote ya kidunia, iwapo hawajapata kuridhika na hali yao.

Pia utamkuta yule asiyetenda kulingana na imani, akijaribiwa na umasikini, au kupoteza baadhi ya matamanio ya kidunia, utamkuta akiwa katika hali ya huzuni na taabu kubwa.

Mfano mwengine ni kwamba zikitokea sababu za hofu, na mtu akapatwa na misukosuko, utamkuta mwenye imani thabiti ana moyo thabiti, nafsi iliyotulia, mwenye uwezo wa kulismamia na kulielekeza jambo hili lililompata kwa yale aliyo nayo na uwezo juu yake kama vile kufikiria, kuzungumza na kutenda.

Yeye tayari alishajizoesha masumbuko haya yanayomsumbu. Kwa hivyo, hali hizi humtulizia mtu moyo wake na kuuimarisha.

Pia utamkuta yule ambaye hana imani akiwa katika hali iliyo kinyume na hiyo. Anapopatwa

na hofu, dhamiri yake inasumbuka sana kwa sababu yake, mishipa yake inakuwa na wasiwasi nyingi, mawazo yake yanatawanyika, na anahisi hofu ya nje na wasiwasi ya ndani ambaao haiwezi kuelezewa ilivyo hasa. Watu wa aina hii, ikiwa baadhi ya sababu za kiasili haziwatokei, ambazo zinahitaji mazoezi mengi, nguvu zao zinaanguka, na mishipa yao inakuwa na wasiwasi; kwa sababu hana imani ambayo husababisha subira haswa katika hali ngumu na hali ya kuhuzunisha na kusumbua.

Mtu mwema na mtu mwovu, Muumini na kafiri, wanashiriki katika kupata ujasiri kwa njia ya kujifunza, na katika silika ambayo hupunguza na kurahisisha hofu. Hata hivyo, Muumini ni tofauti kwa nguvu ya imani yake, subira, kumuamini Mwenyezi Mungu, kumtegemea na kutaraji malipo yake - mambo ambayo yanamzidishia ujasiri, yanampunguzia makali ya hofu na yanamrahisishia matatizo, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلَا تَهُنُّا فِي ابْتِغَاءِ الْقَوْمِ إِنْ تَكُونُوا تَأْلَمُونَ فَإِنَّهُمْ يَأْلَمُونَ كَمَا تَأْلَمُونَ وَتَرْجُونَ مِنَ اللَّهِ مَا لَا يَرْجُونَ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا﴾.

[النساء: 145]

*"Wala msilegee katika kuwafukuzia kaum ya maadui. Ikiwa mnaumia, basi nao pia wanaumia kama mnavyoumia nyinyi. Nanyi mnataraji kwa Mwenyezi Mungu wasiyoyataraji wao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua zaidi, Mwenye hekima."* (An-Nisa: 104).

Pia wanapata msaada maalumu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, usaidizi wa kipekee unaoondoaa hofu zao. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿...وَاصْبِرُوا إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ﴾. [الأنتقال: ٤٥]

*"...na kuweni na subira. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaofanya subira."* (Al-Anfal: 46).

**2-** Na mionganini mwa sababu zinazoondoaa huzuni, dhiki na wasiwasi, ni kutenda viumbe mema kwa kusema na kutenda, na aina zote za wema, na zote hizi ni heri na ihsani. Na kwa njia hii, Mwenyezi Mungu huondoa wasiwasi na dhiki (huzuni) kwa watu wema na watu waovu kulingana na kiwango cha wema wao. Lakini Muumini ana sehemu na fungu kamili zaidi katika hayo, naye ni tofauti kwa kuwa matendo yake mema yanatokana na kumkusudia Mwenyezi Mungu pekee na kutaraji malipo yake.

Hivyo basi, Mwenyezi Mungu humrahisishia kufanya mambo mema kwa sababu ya heri anayotarajia, na humzulia machukizo (matatizo) kwa sababu ya kukusudia kwake Mwenyezi Mungu pekee, na wema wake. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَا حَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّنْ نَجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ وَمَنْ يَفْعُلْ ذَلِكَ ابْتَغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ أُنْوَتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا﴾. [النساء: ١٣٦]

*“Hakuna heri katika mengi ya wanayoshauriana kwa siri, isipokuwa kwa yule anayeamrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi tutakujampa ujira mkubwa.”* (An-Nisaa: 114).

Basi Mwenyezi Mungu Mtukufu alitoa habari kwamba mambo haya yote ni heri kutoka kwa yule ambaye ameyatenda. Na wema huleta wema na huondoa uovu. Na akatoa habari kwamba Muumini anayetarajia malipo kwa Mwenyezi Mungu atapewa ujira mkubwa. Na mionganini mwa malipo hayo makubwa ni kuondolewa wasiwasi, huzuni, dhiki na mengineyo.

## Sura ya Pili

3- Na katika sababu za kuondoa wasiwasi unaotokana na mfadhaiko wa neva na kutetereka kwa neva, na kujishughulisha kwa moyo na mambo yanayohuzunisha ni: Kujishughulisha na matendo fulani au kujifunza elimu yoyote yenye manufaa. Hili linauzuia moyo na kuufanya usiwe na mawazo juu ya jambo lililoupa wasiwasi. Labda kwa sababu ya hayo, anaweza kusahau sababu zilizomletea wasiwasi na huzuni hiyo, hivyo basi nafsi yake ikawa na furaha na ikazidi kuwa na ukakamavu. Muumini na wengineo wanashiriki katika sababu hii. Lakini Muumini anakuwa bora zaidi kwa imani yake, kukusudia kwake Mwenyezi Mungu peke yake na kutajaria malipo kwa sababu ya kujishughulisha kwake na elimu hiyo anayojifunza au anayowafundisha wengine na kwa sababu ya matendo mema ambayo anayafanya. Ikiwa ni ibada, basi inakuwa ibada. Na kama ni shughuli ya kidunia au desturi fulani, anaiambatanisha na nia njema, na akakusudia kuitumia kwenye kujisaidia katika kumtii Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana hilo lina athari ya ufanisi sana katika kuondoa wasiwasi, dhiki na huzuni. Kwani ni watu wangapi

waliopatwa na wasiwasi na dhiki za mara kwa mara, na wakapatwa na magonjwa mbalimbali, basi ikawa dawa yao yenye ufanisi ni kusahau visababu vilivyowatia huzuni na wasiwasi, na pia dawa yao ikawa ni kujishughulisha na kazi miongoni mwa kazi zao muhimu.

Shughuli hii anayoifanya inapaswa kuwa kitu ambacho nafsi yake hupata utulivu ndani yake na kukitamani sana. Kwani, hilo lina uwezekano mkubwa zaidi wa kusababisha kufikia lengo hili lenye manufaa, na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye zaidi.

**4- Na katika mambo anayoweza kujizulia kwayo mifadhaiko na wasiwasi, ni kuelekeza akili yake yote katika kufanya kazi ya siku ya leo, kutojishughulisha kabisa na mambo ya siku zijazo na kutohuzunika juu ya mambo yaliyopita. Ndiyo maana, Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikuwa akijikinga kutokana na wasiwasi na huzuni (katika hadithi iliyosimuliwa na Al-Bukhari na Muslim).**

Kwa sababu kuhuzunika juu ya mambo yaliyopita na ambayo haiwezekani kuyarudisha

wala kuyafikia hakusaidii kitu. Vile vile, huzuni inayotokana na kuhofu mambo ya siku zijazo huenda ikawa na madhara kwa mtu. Hivyo basi, mja anapaswa kuwa mwana wa siku yake, anayekusanya juhudhi na bidii yake katika kuboresha siku yake na wakati wake wa sasa. Kwa kukusanya moyo juu ya hili, itasababisha kukamilika kwa matendo, na itamfariji mja kutokana na huzuni na machungu. Mtume, rehemza amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, anapoomba dua au kuuelekeza Umma wake kwenye dua fulani, hapo huwa anahimiza - pamoja na kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu na kutaraji fadhila zake - juu ya kuichukulia kwa uzito na kufanya bidii katika kufikia anachokiomba kitokee na kuacha yale aliyokuwa akiomba yaondolewe. Kwa sababu dua inafungamana na vitendo.

Na mja anapaswa kujitahidi katika mambo yanayomnufaisha katika dini na dunia, na kumuomba Mola wake Mlezi kwamba afikie lengo lake, na atafute msaada wake katika hilo, kama alivyosema Mtume, rehemza amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

«اَخْرِصْ عَلَىٰ مَا يَنْفَعُكَ، وَاسْتَعِنْ بِاللّٰهِ وَلَا تَعْجِزْ، وَإِنْ أَصَابَكَ شَيْءٌ فَلَا  
تَقْلِنْ: لَوْ أَئِي فَعَلْتُ كَذَا، كَانَ كَذَا وَكَذَا، وَلَكِنْ قُلْ: قَدَرَ اللّٰهُ وَمَا شَاءَ  
فَعَلَ، فَإِنْ لَوْ تَفْتَحْ عَمَلَ الشَّيْطَانِ». (رواه مسلم).

*"Jitahidi katika yenyeye kukunufaisha, na utake msaada kwa Mwenyezi Mungu, wala usikate tamaa. Na likikupata jambo, usiseme: 'Lau ningelifanya hivi, basi ingelikuwa hivi,' lakini sema: 'Mwenyezi Mungu alikwishapanga, naye hufanya akitakacho.' Kwani kusema "Lau" kunafungua matendo ya Shetani."* (Imepokelewa na Muslim).

Hapa, Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikusanya kati ya amri ya kujitahidi katika mambo yenyeye manufaa kwa kila hali na kutafuta msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kutokubali kushindwa, ambako ni kufanya uvivu unaoleta madhara, na baina ya kujisalimisha kwa mambo yaliyopita na kutekelezeka, na kutii mipango ya Mwenyezi Mungu.

Na aligawanya mambo katika sehemu mbili: Sehemu ambayo mja anaweza kujitahidi kupata au kupata anachoweza kutoka kwayo, au

kuizuia au kuipunguza. Sehemu hii, mja anafaa kuonyesha juhudini yake na kutafuta msaada wa Mola wake Mlezi. Na kuna sehemu ambayo hawezizaji kufanya hivyo. Sehemu hii, mja anafaa kutulizana, kuridhia na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu. Hakuna shaka kwamba kuzingatia kanuni hii ni sababu ya furaha na kuondoka kwa wasiwasi na huzuni.

## Sura ya Tatu

5- Na katika sababu kubwa za kufunguka kwa moyo na utulivu wake ni kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi, kwani hilo lina athari ya ajabu katika kufunguka na utulivu wa moyo, na kuondoka kwa wasiwasi na huzuni yake. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

...أَلَا يَذِكُرِ اللَّهُ تَطْمِئْنُ الْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾ [الرعد: 28].

*"Kumbukeni, hakika kwa kumtaja Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hupata utulivu."* (Ar-Ra'd: 28).

Kumtaja Mwenyezi Mungu kuna athari kubwa katika kufikia lengo hili kutokana na sifa zake maalumu, na kwa sababu ya malipo na thawabu zake ambazo mja anazitarajia.

**6-** Vile vile, kuzungumzia neema za Mwenyezi Mungu za ndani na za nje. Kuzijua na kuzizungumzia kunachangia Mwenyezi Mungu kuondoa wasiwasi na huzuni, na kunamhimiza mja kushukuru, jambo ambalo ndilo daraja la juu kabisa na tukufu, hata kama mja yuko katika hali ya ufukara, magonjwa au aina nyingine za misiba. Kwa maana ikiwa atalinganisha neema za Mwenyezi Mungu juu yake - ambazo hazihesabiki - na matatizo yaliyompata, basi matatizo hayo hayataweza kulinganishwa hata kidogo na neema hizo.

Bali Mwenyezi Mungu akimjaribu mja kwa matatizo na balaa, na akatekeleza wajibu wa subira, kuridhika, na kujisalimisha, basi athari yake inakuwa nyepesi, mzigo wake unakuwa hafifu, na tumaini la mja la kupata malipo yake na thawabu zake na kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa kutenda wajibu wa subira na kuridhika humfanya kuhisi vitu vichungu vitamu, na utamu wa malipo yake humfanya asahau uchungu wa subira yake.

**7-** Na miongoni mwa mambo yenye manufaa makubwa zaidi katika hali hii ni kutumia yale aliyotuongoza kwayo Mtume, rehema na

amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, katika Hadithi Sahihi pale aliposema:

«انْظُرُوا إِلَى مَنْ هُوَ أَسْفَلُ مِنْكُمْ، وَلَا تَنْظُرُوا إِلَى مَنْ هُوَ فَوْقُكُمْ، فَهُوَ أَجْدَرُ أَنْ لَا تَرْدَرُوا بِنِعْمَةِ اللَّهِ عَلَيْكُمْ». (رواه البخاري).

*"Watazameni wale walio chini yenu na msiwaangalie wale walio juu yenu. Hilo litawafanya zaidi kutodharau neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu."* (Imepokelewa na Al-Bukhari).

Ikiwa mja ataweka maono haya makubwa mbele ya macho yake, utamuona akishinda idadi kubwa ya watu katika kuwa salama na katika kufikia manufaa yanayoambatana na hilo, na katika riziki na yanayoambatana nayo, bila kujali ni kiwango gani hali yake imemfikisha. Basi unaondoka wasiwasi wake na huzuni yake, na furaha na bashasha yake vinazidi kwa sababu ya neema za Mwenyezi Mungu, ambazo aliwazidi kwazo wengine walio chini yake.

Na kila kunavyozidi kutafakari kwa mja neema za Mwenyezi Mungu za nje na za ndani, za kidini na za kidunia, ndivyo anavyoona zaidi kwamba Mola wake Mlezi amempa heri na kumuepusha na maovu mengi. Na hakuna

shaka kwamba hilo linazuia wasiwasi na huzuni,  
na linaleta furaha na bashasha.

## Sura ya Nne

**8-** Na mionganini mwa sababu ziletazo furaha na kuondoa wasiwasi na huzuni ni kujitahidi kuondoa sababu zinazoleta wasiwasi na kutafuta sababu zinazoleta furaha.

Hilo linakuwa kwa kusahau shida zilizopita ambazo hangeweza kuziepuka, na kujua kwamba kuishughulisha akili yake katika hayo ni kazi bure na kitu kisichowezekana, na kwamba huo ni upumbavu na ni jambo lisilowezekana. Kwa hivyo, na apambane na moyo wake dhidi ya kufikiria juu yake, na pia apambane na moyo wake dhidi ya kuwa na wasiwasi juu ya mambo yajayo, ikiwa ni pamoja na umasikini, hofu au mambo mengineyo mionganini mwa machukizo ambayo anadhani kwamba yatampata katika maisha yake yajayo.

Anapaswa kujua kwamba mambo yajayo hayajulikani ni nini kitakachotokea cha heri na shari, matumaini na machungu, na kwamba yamo mikononi mwa Mwenye nguvu, Mwenye hekima. Waja hawana uwezo

juu yake isipokuwa kujitahidi kupata heri zake na kuzuia madhara yake. Na mja anapaswa pia kujua kwamba ikiwa atageuza mawazo yake kutoka kwenye wasiwasi wake kwa ajili ya maisha yake yajayo, na kumtegemea Mola wake Mlezi katika kuyafanya yatengenee, na akapata utulivu kwake katika mambo hayo, akifanya hayo moyo wake utatulia, hali zake zitakuwa bora na huzuni wake na wasiwasi utaondoka.

**9-** Na miiongoni mwa mambo yenyeye manufaa makubwa zaidi katika kuutazama mustakbali wa mambo, ni kutumia dua hii ambayo Mtume, rehemaa na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikuwa akiomba kwayo:

«اللَّهُمَّ أَصْلِحْ لِي دِينِي الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي، وَأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ الَّتِي  
فِيهَا مَعَاشِي، وَأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي الَّتِي إِلَيْهَا مَعَادِي، وَاجْعَلْ الْحَيَاةَ زِيادةً  
لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ، وَالْمَوْتَ رَاحَةً لِي مِنْ كُلِّ شَرٍ». (رواه مسلم).

*"Ewe Mwenyezi Mungu, nitengenezee dini  
yangu ambayo ndiyo kinga ya mambo yangu.  
Na nitengenezee dunia yangu ambayo  
kunapatikana maisha yangu. Na nitengenezee  
Akhera yangu ambako ndiko nitakakorejea. Na  
fanya maisha yangu kuwa nyongeza ya kheri*

*kwa kila jambo jema, na kifo kiwe pumziko kwangu kutoka kwa kila shari.*" (Imepokelewa na Muslim).

Na pia kauli yake, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

«اللَّهُمَّ رَحْمَتَكَ أَرْجُو، فَلَا تَكِلْنِي إِلَى نَفْسِي طَرْفَةَ عَيْنٍ، وَأَصْلِحْ لِي شَأْنِي كُلَّهُ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ» . (رواه أبو داود بسناد صحيح).

*"Ewe Mwenyezi Mungu, rehema yako ndiyo ninayotarajia, wala usiniache nijisimamie mwenyewe kiasi cha kupepesa kwa jicho, na rekebisha kila jambo langu, hakuna mungu isipokuwa Wewe."* (Imepokelewa na Abu Daawuud kwa msururu mzuri wa wasimulizi).

Hivyo basi, ikiwa mja atasema dua hii ambayo ina manufaa ya maisha yake ya kijumla ya kidini na ya kidunia kwa moyo thabiti, na nia ya dhati, pamoja na juhudhi yake katika kutimiza hayo, Mwenyezi Mungu atamjalia aliyoyaomba na alivyotarajia, na huzuni yake itageuka kuwa furaha na shangwe.

## Sura ya Tano

**10-** Na mionganoni mwa sababu zenyeye manufaa zaidi za kuondoa wasiwasi na huzuni iwapo mja

atapatwa na baadhi ya matatizo, ni kujitahidi kuyapunguza kwa kukadiria matokeo mabaya zaidi ambayo jambo hilo linaweza kufikia, na aizoeshe nafsi yake kwa hilo. Akifanya hivyo, basi na ajitahidi kupunguza yale yanayoweza kupunguzwa kiasi inavyowezekana.

Kwa kujzoesha huku, na kwa juhudii hii yenye manufaa, utaondoka wasiwasi wake na huzuni yake, na atakuwa amefanya bidii hiyo katika kuleta manufaa na kuzuia madhara ambayo ni rahisi kwa mja.

Kwa hivyo, anapopatwa na sababu za hofu, sababu za maradhi, sababu za umasikini na ukosefu wa vitu mbalimbali anavyopenda, basi na ayapokee hayo kwa utulivu na kujzoesha juu yake. Bali anafaa kufanya hivyo juu ya lililo kali zaidi mionganoni mwake. Kwani kuizoesha nafsi kustahimili matatizo, huyafanya yawe rahisi na huondoa ukali wake, haswa ikiwa atajishughulisha na kuyazuia kulingana na uwezo wake.

Hapo yatakuwa yamekusanyika kwake kuizoesha nafsi pamoja na kufanya bidii yenye manufaa ambayo yamatshughulisha mbali na kujali balaa hizo, na atajitahidi kufanya upya nguvu ya kuzuilia balaa hizo, huku akimtegemea

Mwenyezi Mungu katika hilo na kuwa na imani nzuri naye.

Na hakuna shaka kwamba mambo haya yana manufaa makubwa sana katika kuleta furaha na kufunguka kwa nyoyo, pamoja na yale anayoyatarajia mja ya malipo ya sasa na ya baadaye. Hili ni jambo ambalo limeshuhudiwa na kujaribiwa, na matukio yake kwa wale waliolijaribu ni mengi sana.

## Sura ya Sita

**11-** Na mionganoni mwa tiba kubwa zaidi ya magonjwa ya moyo ya neva, na hata kwa magonjwa ya kimwili, ni nguvu ya moyo na kutosumbukana, kuathirika na dhana na mawazo yanayoletwa na fikira mbaya. Hasira na kuchanganyikiwa ni mionganoni mwa sababu zinazoumiza. Na mwenye kutarajia kutokea kwa machukizo na kutoweka kwa mambo anayoyapenda, mara hayo humsababishia wasiwasi, huzuni na magonjwa ya kimoyo na ya kimwili, na kuzorota kwa neva, ambako kuna athari zake mbaya, ambazo watu wameshuhudia madhara yake mengi.

**12-** Na pindi moyo unapomtegemea na kuyakabidhi mambo yake kwa Mwenyezi Mungu, na usijisalimishe kwa mawazo yasiyo ya kweli wala usimilikiwe na fikira mbaya, na ukawa na imani na Mwenyezi Mungu na ukatulizana juu ya fadhila zake, wasiwasi na huzuni wake zitawekwa mbali sana na yeye kwa sababu ya hayo na yatamwondoka maradhi mengi ya kimwili na kimoyo, na moyo wake utapata nguvu, utafunguka na atakuwa na furaha ambayo haiwezi kuelezeaka.

Je, ni hospitali ngapi zilizojaa wagonjwa wanaoteseka kutokana na msongo wa mawazo na fikira mbovu? Na je, ni wangapi miongoni mwa watu wenye nguvu walioathirika na mambo haya, mbali na watu wanyonge? Na ni mara ngapi mambo haya yemesababisha upumbavu na wazimu? Basi aliye salama ni yule ambaye Mwenyezi Mungu amempa salama, na akamuwezesha kupambana na nafsi yake ili kupata visababu vyenye manufaa, vya kuuimarisha moyo, vya kuzuia wasiwasi wake. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿...وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ...﴾. [الطلاق: ٣].

*"Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, basi Yeye humtosha."* [At-Twalaq: 3].

Yaani, atamtosheleza katika mambo yote ya dini yake na dunia yake yanayompa wasiwasi.

Anayemtegemea Mwenyezi Mungu ana moyo wenyewe nguvu, haathiriwi na mawazo yasiyo ya kweli, na hasumbuliwi na matukio, kwa sababu anajua kwamba hili ni katika udhaifu wa nafsi, na ni katika udhaifu na hofu ambayo haina uhakika, na anajua kwamba Mwenyezi Mungu amemdhaminia utoshelevu kamili yule anayemtegemea. Kwa hivyo anakuwa na imani na Mwenyezi Mungu na anatulizana juu ya ahadi yake, kwa hivyo unaisha huzuni wake na wasiwasi wake, kisha ugumu wake huo unabadijika kuwa wepesi, na huzuni wake unakuwa furaha, na hofu yake inakuwa amani.

Kwa hivyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu salama, na atujaalie kutokana na fadhila zake, nguvu na uthabiti wa moyo, na kumtegemea kikamilifu ambako Mwenyezi Mungu amewahakikishia watu wake kwamba

watapata kila heri, na wataepushwa kila machukizo na madhara.

## Sura ya Saba

**13-** Kuna faida mbili kuu katika kauli ya Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

«لَا يَفْرُكُ مُؤْمِنٌ مُّؤْمِنَةً، إِنْ كَرِهَ مِنْهَا حُلْقًا رَضِيَ مِنْهَا آخَرٌ». (رواہ مسلم).

*"Mwanamume Muumini asimchukie mwanamke Muumini. Iwapo atachukia tabia moja kutoka kwake, ataridhika na nyininge."* (Imepokelewa na Muslim).

**Faida ya kwanza:** Mwongozo wa jinsi ya kuamiliana na mke, jamaa, rafiki, na mfanyakazi na kila mtu ambaye una uhusiano na mawasiliano naye, na kwamba unapaswa kuwa umetayarisha nafsi yako kwamba lazima atakuwa na kasoro au upungufu au kitu unachokichukia. Kwa hivyo, ukipata hicho, basi linganisha hiki na kile kinachotakiwa kwako au unachopaswa kufanya cha kuwa na mawasiliano ya nguvu na kudumisha upendo, kwa kukumbuka mazuri yake, na madhumuni mahususi na ya ujumla. Basi kwa kupuuza makosa hayo na kutambua mazuri

yao, unadumu usuhuba na mawasiliano na utapata utulivu na faraja.

**Faida ya pili:** Ni kuondoka kwa huzuni na wasiwasi, kubaki kwa upole, na kuendelea kutekeleza haki za lazima zilizopendekezwa, na kupatikana kwa faraja baina ya hizi pande mbili. Kwa hivyo, asiyechukua mwongozo huu alioutaja Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, badala yake akageuza jambo hili na akaangalia mabaya tu, na akapuuza mazuri, basi lazima atakuwa na wasiwasi, na lazima kutakuwa na mahusiano mabaya kati yake na mtu aliyekuwa ameunganishwa naye kwa upendo, na kutakuwa na kukatwa kwa haki nyingi ambazo kila mmoja wao anapaswa kuzihifadhi.

Na watu wengi wenye ari ya juu hujianaa kiakili wakati wa majanga na shida kwa subira na utulivu. Lakini wakati wa mambo madogo na yasiyokuwa na maana, wanahisi wasiwasi, na furaha yao inakuwa na dhiki. Sababu ya hili ni kwamba walijizatiti mbele ya mambo makubwa, lakini walijisahau kwenye mambo madogo, kwa hivyo ikawaathiri na kuathiri faraja yao.

Mtu mwenye busara hujiandaa kwa mambo yote, makubwa na madogo, na anamuomba Mwenyezi Mungu msaada juu yake, na asimwache mwenyewe hata kwa sekunde moja. Hivi ndivyo atakavyoweza kukabiliana na mambo madogo kwa urahisi, kama vile alivyoweza kushughulikia mambo makubwa Kwa hivyo, anabaki akiwa ana utulivu wa nafsi, utulivu wa moyo na kuhisi faraja.

## Sura ya Nane

**14-** Mwenye busara anajua kuwa maisha yake bora ni maisha ya furaha na utulivu, na kwamba ni mafupi sana, basi hafai kuyafupisha kwa wasiwasi na kujiingiza kwenye mahangaiko, kwani, hilo ni kinyume na maisha sahihi. Kwa hivyo, anayafanyia choyo maisha yake ili sehemu kubwa yake isitwaliwe bure tu na mawazo mabaya na huzuni. Katika hili, hakuna tofauti kati ya mtu mwema na muovu, lakini Muumini anasifika zaidi na sifa hii na ana fungu na sehemu kubwa zaidi yenye manufaa ya sasa na ya baadaye katika hilo.

**15-** Pia inafaa anapopatwa na msiba au ikiwa atauhofu, basi na alinganishe kati ya neema alizo nazo, ziwe ni za kidini au za kidunia, na kati

ya msiba uliompata. Akilinganisha, zitakuwa wazi neema alizo ndani yake na utapotelea mbali msiba huo uliompata.

Vile vile, alinganishe kati ya madhara anayoyahofu kumtokea na uwezekano mwingi wa kuwa salama kutokana nayo. Hapo asiache uwezekano dhaifu ushinde uwezekano mwingi wenye nguvu, na kwa hilo utaondoka wasiwasi wake na hofu yake.

**16-** Na anafaa kukadiria uwezekano mkubwa zaidi unaoweza kumpata. Hali hiyo humuwezesha kijiandaa kwa ajili ya kitakachotokea, na pia kutafuta kuzuia kile kisichotokea na kuboresha au kupunguza kile kilichotokea.

**17-** Na mionganoni mwa mambo yanayofaa ni kujua kwamba madhara yatokanayo na watu kwako, hasa kwa maneno mabaya, hayakudhuru bali yanawadhuru wao wenyewe, isipokuwa ikiwa utajishughulisha nayo na kuyaruhusu yazimiliki hisia zako. Hapo ndipo yatakavyokudhuru kama yalivyowadhuru wao. Lakini ikiwa hutayapa kipaumbele, basi hayatakudhuru kwa chochote.

Jua ya kwamba maisha yako yanategemea fikira zako. Ikiwa ni fikira zenye manufaa kwako katika dini au katika dunia hii, basi maisha yako ni mazuri na yenye furaha. Vinginevyo, ni kinyume chake.

**18-** Na mionganini mwa mambo yenye manufaa zaidi katika kuondoa wasiwasi, ni kujizoesha kutotafuta shukrani isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, ukimfanyia wema mtu ambaye ana haki juu yako au asiyekuwa na haki juu yako, jua ya kwamba hapo unaamiliana na Mwenyezi Mungu. Basi usijali kuhusu shukrani za wale uliowafanyia wema, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu viumbe wake maalumu:

﴿إِنَّمَا نُظْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا تُرِيدُ مِنْكُمْ جَرَاءً وَلَا شُكُورًا﴾.

[الإنسان: ١]

*"Hakika sisi tunakulisheni kwa ajili ya uso wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani."* [Al-Insan: 9].

Hili linasisitizwa zaidi katika kuamiliana na mke, watoto wako, na kwa sababu ya nguvu

ya uhusiano wako nao. Kwa hivyo, pindi unapojizoesha kuwaondolea ubaya, basi utakuwa umeshajipumzisha. Miongoni mwa vyanzo vya utulivu ni kuchukua fadhila na kuzitekeleza kulingana na hamu ya ndani, bila kujilazimisha kwa jambo linalokusumbua. Kwani hivyo unaweza kurudi nyuma ukiwa umeshindwa kupata fadhila, baada ya kuchukua njia ndefu isiyokuwa na manufaa. Hilo ni hekima. Pia unafaa kuchukua mambo safi na matamu kutoka kwa mambo mabaya, na kwa hilo utazidi usafi wa kidhati, na yataondoka mambo machafu.

Weka mambo ya manufaa mbele yako na fanya juhudini kuyafikia, wala usigeukie mambo yenye madhara ili kujifurahisha kwayo mbali na sababu zinazosababisha wasiwasi na huzuni. Tumia utulivu na umoja wa nafsi katika kutekeleza kazi muhimu.

**19-** Na miongoni mwa mambo ya manufaa, ni kumaliza kazi kwa wakati, na kujitolea kwa kazi zijazo. Hii ni kwa sababu kazi ambazo hazikamiliki hukusanya kazi zingine zilizopita, na kuongezeka kwa kazi zijazo, na kufanya mzigo kuwa mzito. Lakini ikiwa utamaliza kila

kitu kwa wakati, utakutana na kazi zijazo kwa nguvu ya mawazo na nguvu ya kutenda kazi.

**20-** Unapaswa kuchagua vitendo vyenye manufaa; muhimu zaidi kisha muhimu zaidi, na upambanue kati ya kile ambacho nafsi yako inakielekea na kile unachotamani sana, kwa sababu kinyume chake husababisha kuchoshwa, uchovu na huzuni. Tafuta msaada katika hili kwa kufikiri kisahihii na kushauriana. Kwani, hatajuta kamwe mwenye kutafuta ushauri.

Soma kwa uangalifu kile ambacho unataka kukifanya. Kwa hivyo, ikiwa kina masilahi, na ukakiazimia, basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaomtegemea.

**21-** Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Na rehemaa na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya bwana wetu Muhammad, familia yake na Maswahaba wake.

## **Yaliyomo**

Utangulizi wa Mwandishi .....	1
Sura ya Kwanza .....	2
Sura ya Pili.....	11
Sura ya Tatu .....	15
Sura ya Nne.....	18
Sura ya Tano .....	20
Sura ya Sita .....	22
Sura ya Saba.....	25
Sura ya Nane .....	27



رَسَالَةُ اللَّهِ الْحَرَمَانِ

# Ujumbe wa Haramain

Maudhui ya mwongozo kwa wanaokusudia Msikiti wa Haram na  
Msikiti wa Nabawi kwa lugha.



**978-603-8517-75-8**